

# UFADHILI WA WAKIMBIZI

MPYA

Kwa mara ya kwanza kwa miaka arobaini, **vikundi vya Wamarekani wowote** wanaweza kutoa ufadhili wao wenyewe kwa wakimbizi nchini marekani kwa kutumia kielelezo kilichotolewa kutoka kwa mpango wa Kanada wa “Kikundi cha watu 5” inayoitwa Mpango wa Welcome Corps.

## HIAS ina vidokezo 5 vya kuunda kikundi cha wafadhili kilichofaulu

1

### ZIFAHAMU AWAMU

**Awamu ya 1 (inaendelea sasa):** serikali ya Marekani itawakutanisha wafadhili na wakimbizi wasiowajua. Hapo awali, wakimbizi kutoka Kusini mwa Sahara Barani Afrika wangezingatiwa.

**Awamu ya 2 (katikati hadi mwishoni mwa 2023):** wafadhili wanaweza kutambua wakimbizi wanambao wangetaka kufadhili.

**Unaweza kuanza kujipanga kwa awamu ya 2 sasa!**

2

### UNDENI KIKUNDI CHENU

Utahitaji angalau **watu 5 ili kuunda kikundi cha ufadhili**. Wafadhili wanahitajika:

- Wawe na umri wa zaidi ya miaka 18
  - Wapite ukaguzi wa usuli
  - Watie saini kanuni za maadili
- Kupokea mafunzo yatakayotolewa mtandaoni
- Kuishi katika eneo ambapo wakimbizi wataishi.

3

### KUCHANGISHA PESA

**HIAS inaweza kukusaidia kujua kiasi cha pesa ngapi utakachohitaji.**

Serikali inakuhitaji uchangisha dola 2,425 kwa kila mkimbizi anayefadhiliwa. Hata hivyo, gharama halisi (ikiwa ni pamoja na kulipa kodi ya nyumba, chakula, huduma za wakimbizi, na zaidi) hutofautiana kutoka jimbo moja hadi lingine.

4

### MPANGO WA UKARIBISHAJI

**Utahitaji kuandika “Mpango wa Ukaribishaji”** unaoonyesha jinsi utakavyotoa huduma za msingi za uhamiaji kama vile kuwachukua kutoka uwanja wa ndege, kuwatafutia makazi salama, kuwasajili kwa manufaa ya umma, kuwatafutia kazi, na zaidi.

**Usiwe na hofu, HIAS inaweza kusaidia katika hatua hii!**

5

### WASILIANA NA HIAS

**HIAS ina zana, nyenzo na uzoefu wa kukuongoza** katika mchakato wote wa kutuma maombi, kupata washirika na kuunga mkono safari yako ya ufadhili.

Pata maelezo zaidi katika [hias.org/welcome-circles](https://hias.org/welcome-circles)  
Barua pepe [info@hias.org](mailto:info@hias.org)

Piga simu kwa 800-HIAS-714  
(800-4427-714)



Welcome the stranger.  
Protect the refugee.